Mzee Ibrahimu

Kitabu cha Mwanzo tena, sura ya 22, kuanzia aya ya 15, na tunatazamia sasa kuzungumza tu kwa muda mchache na kuanza ibada. Mwanzo 22, kuanzia na aya ya 15.

> *Malaika wa* BWANA *akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni,*
>
> *Akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu, asema* BWANA, *kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao pekee:*
>
> *Katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao;*
>
> *Na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu.*

2 Ni ahadi kuu jinsi gani, kwa sababu ya utii! Utii ndio Mungu atakao. Ilinenwa wakati mmoja, "Kutii ni bora kuliko dhabihu." Kumtii Bwana ni bora kuliko dhabihu yo yote ungeweza kutoa.

3 Tunakabili sasa somo muhimu mno, usiku wa leo, *Mzee Ibrahimu,* ambaye aliitwa "baba wa Imani," kwa sababu kwamba Mungu alimpa ahadi kuirithi nchi, na Uzao wake. Na ni kwa kupitia Ibrahimu sisi, tulio wafu katika Kristo, tunakuwa Uzao wa Ibrahimu na warithi pamoja na Yeye kulingana na ile ahadi.

4 Sasa, Ibrahimu alikuwa mtu wa kawaida tu, hakuwa kitu maalum. Mungu hakumwita kamwe, kadiri tulivyo na kumbukumbu yake, hadi alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano. Mkewe, ambaye, alikuwa dada wa kuchangia mzazi, akiwa na miaka sitini na mitano wakati huo, labda waliishi pamoja tangu walipokuwa vijana sana. Naye alikuwa tasa, na hakuwa na watoto. Mungu aliagiza utengano kamili, kujitenga wenyewe na ulimwengu, na watu wake wote, na jamaa yake yote. Kulikuwa na jambo maalum kwa yeye kutenda.

5 Na wakati Mungu anapokutazamia wewe kutenda jambo maalum, Yeye hutaka ujitenge kabisa na shaka yo yote. Yakubidi ufikie utii mkamilifu, kutii asemalo. Mungu hulitaka hilo. Huwezi ukalitenda kwa njia nyingine. Na, sasa, Yeye sikuzote huweka mfano, na huo ulikuwa mfano Wake, wa kujitenga kabisa na familia yake yote, jamaa yake yote, na kadhalika, kutembea katika maisha yaliyotengwa kwa Mungu.

6 Miaka ilipita, hakuna kilichotukia, lakini bado Ibrahimu aliendelea kushikilia. Hakushushwa moyo. "Hakusita kamwe

kwa zile ahadi za Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu."

7 Mwaka baada ya mwaka, kadiri ilivyopita, bila shaka watoa lawama wengi walikuja wakasema, "Ibrahimu, baba wa mataifa, unao watoto wangapi sasa?" Hilo halikumfanya asite. Bila mtoto, naye Sara alikuwa amepita wakati wa maisha, wa kuzaa watoto, bila shaka, alipita wakati wa kupata hedhi siku nyingi sana, hata hivyo Ibrahimu alimwamini Mungu sawasawa tu. Alifanya maandalizi ya mtoto, kwa sababu alijua hakika kabisa kwamba Mungu asingetoa ahadi ambayo Yeye si mkuu vya kutosha kuitekeleza.

8 Uzao Wake wapaswa kufikiria kitu kile kile. Haidhuru jinsi gani haielekei kuwa kweli, jinsi ionekanayo isiyo ya kawaida kwa akili ya kiasili, hata hivyo Mungu hawezi kufanya ahadi ambayo Yeye si mkuu vya kutosha kuishughulikia. Tunaamini jambo lilo hilo hivi leo. Kila Mzao wa kweli wa Ibrahimu huamini jambo lilo hilo. Haidhuru hali ilivyo, tumeongeza maarifa kiasi gani, mambo mangapi yametukia, jinsi gani isivyoonekana ya kawaida kwa nia ya asili, ni la kipuzi namna gani, hasa, kwa nia ya asili, haileti tofauti hata chembe. Kama Mungu alinena hivyo, ndivyo ilivyo. Na Uzao wa Ibrahimu umetulia katika BWANA ASEMA HIVI. Hilo latosha.

9 Twaona, kwenye miaka ishirini na mitano baadaye, hakuna watoto. Na bado Mungu alikuwa mwaminifu kudumisha ahadi Yake kwa Ibrahimu, kwa maana Ibrahimu alimwamini Mungu. Mvulana mdogo akatokea, mtoto Isaka.

10 Basi baada ya mtoto Isaka kutokea, ndipo tunaona kwamba Mungu alimpa jaribio maradufu. Yeye akasema, "Mtoto huyu. . . " Baada ya kuwa sasa kama miaka mia moja na kumi na mitano, au ishirini, Ibrahimu alikuwa hivyo. Akasema, "Nataka wewe umchukue huyu, mwanao wa pekee, ukaende zako mpaka kwenye mlima ambao nitakuonyesha, na huko umtoe sadaka, kwenye mlima huu, kama dhabihu." Kwa maneno mengine, aharibu kila ushahidi aliokuwa nao kwamba ile ahadi ingetimizwa. Huko ni kuondoa mambo yote ya asili.

11 Naye Ibrahimu akasema, "Nilimpokea kama mmoja katika wafu. Nami nina hakika kabisa kwamba Yeye aweza kumfufua katika wafu."

12 Hao ndio watu sasa Uzao wa Ibrahimu, kwa sababu Yeye alitufufua katika wafu. Tulikuwa tumekufa katika dhambi na makosa. Na Yeye Ambaye aliweza kubadili nia yangu, kubadili mawazo yangu, kubadili asili yangu, kunibadili kabisa kila mahali, Yeye aweza kutenda apendavyo. Cho chote Yeye asemacho, ninaamini ni Ukweli, na kila Mzao wa Ibrahimu huamini kitu kile kile.

13 Ibrahimu, bila kumuasi Mungu, alimchukua yule mvulana mdogo. Na mnamo asubuhi hii, aliwaambia watumishi, "Ninyi

subirini hapa na nyumbu. Nami pamoja na mwanangu tutaenda kule kuabudu, kisha mimi naye tutarudi.” Loo, anakwenda kulitenda hilo namna gani? Anapopanda mlimani, kuutoa uhai wa mwanawe, hata hivyo anasema, “Mtoto, mimi na mvulana huyu tutarudi.” Alijua kwamba jambo fulani lapaswa litukie. Naye hakujua tu jinsi gani Mungu yuaenda kulitenda hilo; hilo si swali lake. Anajua kwamba Mungu aliahidi hilo.

14 Hilo ndilo lote tunalojali kujua, Mungu aliliahidi! Itakuwaje? Siwezi kuwaambia. Bali Mungu alisema hivyo! Yeye atampeleka Yesu Kristo, mara ya pili, atakuja katika mwili. Atadai Walio Wake. Kutakuwa na miaka elfu moja, Utawala wa Miaka Elfu Moja juu ya dunia hii, pamoja na Yeye, na waliokaombolewa. Hilo ndilo aliloahidi, na tunatazamia saa hiyo ije.

15 Yeye aliahidi kuwaponya wagonjwa, kufufua wafu, kutoa pepo. Yeye aliahidi kufanya hilo. Yeye ni yeye yule jana, leo na hata milele. Jinsi gani? Sijui. Yeye aliahidi kulitenda! Tunaliamini; hilo latosha. Mtu anapomwamini Mungu, huamini yote Yeye asemayo.

16 Na hivyo ndivyo Ibrahimu alivyomwamini Mungu. Sasa aliambiwa aharibu kila ushahidi kwamba ahadi Yake ingeshughulikiwa, lakini alihakikishiwa kwamba Mungu angeweza kulitenda.

17 Sasa, Yeye hakumpa ahadi hii kuu tu, Yeye aliitoa kwa Mzao wake, pia. Na kwa sababu Ibrahimu alikuwa mwaminifu, na alishika Ne—Neno la Mungu ambalo Mungu alimwahidia yeye, na alijua kwamba Mungu angeweza kumfufua mtoto huyu. Basi yeye hakumhurumia mwanawe; lakini (Mungu) alikuwa mfano wa Mungu akimtoa Mwanawe, bila shaka; alipokuwa amebeba kuni akipanda mlima, na kadhalika; kama Kristo baadaye alivyobeba gogo Lake Mwenyewe la sadaka, akakwea kilimani, ambapo alisulubiwa.

18 Tunatambua kwamba katika hili, katika kutenda hili, ilimpendeza sana Mungu kuona kwamba Ibrahimu alimpenda zaidi ya kila kitu duniani, hata mwanawe wa pekee. Alimpenda zaidi ya ambalo mtu ye yote angeweza kusema, mtu ye yote angefanya, bado alimpenda Mungu vya kutosha kuamini Neno Lake.

19 Uzao wote wa Ibrahimu humwamini Mungu namna hiyo. Wanamwamini Mungu. Na twajua kwamba ilimpendeza Mungu sana hata haya ndiyo Yeye aliyosema, “Uzao wako utamiliki malango ya adui zao. Uzao wako utamiliki malango ya adui zao.” Kumbuka, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Uzao wa Ibrahimu huamini hilo. Kama wewe u Mzao halisi wa Ibrahimu, imani ile ambayo Ibrahimu alikuwa nayo katika Mungu, imo ndani yako. Nawe unaamini, kwamba Mungu alilosema, Mungu hutimiza ahadi Yake.

20 Na Yeye alisema hivyo, sasa kumbuka, Yeye alifanya tu ahadi hii kwa Ibrahimu baada ya Yeye kumpa jaribio. Uzao wa Ibrahimu lazima kwanza ujaribiwe, kuona kama kweli wanaamini Neno. Kumbuka, njia ya pekee ambayo angeweza kushikilia ahadi ya Mungu, kwa sababu aliamini ahadi ya Mungu, naye alijaribiwa kama aliiamini au la.

21 Tunafikishwa kwenye jaribio hilo. Uzao wa Ibrahimu, leo, unafikishwa kwenye jaribio hilo. Je, tutachukua Neno la Mungu, au tunachukua ambalo mwanadamu amesema kuhusu hilo Neno? Je, tutachukua ambalo madhehebu fulani yametengeneza kama kanuni ya imani, na kukubali hilo, au tunachukua ambalo Mungu amesema? Kama Neno la Mungu ni kweli, tunaamini Neno la Mungu, bila ya kujali kitu cho chote kile. Tuache kila neno la mwanadamu liwe uwongo, na la Mungu liwe Ukweli. Uzao wa kweli wa Ibrahimu! Lakini kabla ya wewe kuwa huo Mzao wa kweli, yakubidi kupitia katika jaribio, kama alivyofanya Ibrahimu, mwenywewe. Yeye hakumwahidi Ibrahimu pekee, bali Uzao wake ungemiliki malango ya adui. Loo, jamani!

22 Fikiria tu, yule mzee alikuwa amehakikishiwa katika hilo, katika jaribio lake la ahadi ya Neno la Mungu, lilikuwa sahihi. Bila ya kujali hali ilivyokuwa, bado yeye aliamini Neno ni kweli. Yule Ibrahimu, yule mzee maarufu, hakusita katika imani, alipofikishwa kwenye wakati ule wa kujaribiwa. Aliamini kwamba Mungu aliweza kumfufua katika wafu. Aliamini hilo, kwa sababu Mungu aliahidi. Na hapo Mungu alipofanya ahadi kwamba angekuwa "baba wa mataifa," na aliamini kwamba hilo lilikuwa hivyo. Hakujua jinsi gani lingekuwa. Mtoto mchanga alipokuja, baada ya kuamini, miaka ishirini na mitano, ndipo akaambiwa amwangamize yule mtoto, bado alijua kwamba ahadi ya Mungu ilikuwa kweli, naye akamtoa mwanawe.

23 Mzao Wake, jambo lile lile! Ahadi ya Mungu ni muhuri, kwa wale ambao ni Uzao wa Ibrahimu. Ahadi ni muhuri, ushahidi uliotiwa sahihi. Nasi tunapoamini kila Neno lililoahidiwa, basi muhuri unatolewa kwetu, kuthibitishia ahadi kwake. Mnaona, kama sisi—kama sisi, tukiwa Uzao wa Ibrahimu, twapitishwa majaribuni kuona kama tutaamini Biblia, au la. Biblia ni Neno la Mungu, kwa sababu ni Mungu. Na basi baada ya kupitia majaribuni, kuamini.

24 Wakati baadhi yao wasemapo, "Siku za miujiza zimepita." Kama ukikubali hilo, hilo ni kinyume cha Neno.

25 Kama ukisema, "Humpokei Roho Mtakatifu, leo. Hakuna kitu kama hicho. Ni wale mitume kumi na wawili pekee waliompokea."

26 Neno lilisema, Petro akihubiri Hilo siku ya Pentekoste, alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea

kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

27 Hivyo ndivyo Hilo linavyomaanisha hasa. Ni, sasa kama uko tayari kujaribiwa, na jaribio la Mungu la kuhakikisha kabisa, na kufuatilia amri ya daktari, ninakuambia utaona kwamba Mungu hutimiza Neno Lake, kama utaliamini. Hiyo ni kweli. Bali yakubidi upitie katika hayo, kwa sababu huo ndio muhuri; unapoweza kuupokea, basi utapokea ile ahadi. Kwa sababu, Hilo ndilo agizo la Mungu, namna itupasavyo kulifuata Hilo, na hivyo ndivyo itupasavyo sisi kukifuata, kile tu alichosema Yeye. Sasa si kwa baadhi yao tu, bali "ye yote," ye yote aaminiye, ye yote atubuye, ye yote aaminiye. Ni kwa vizazi vyote, kwa watu wote, ye yote atakaye kuamini. Na imani katika Neno la Mungu hukuleta kwenye ahadi hii. Basi hapo, na hapo tu, ndipo unaweza kuwa na nguvu kumiliki muhuri wa ahadi ile.

28 Na ahadi ambayo tunapokea, ule muhuri, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Kwa maana huyo ni Mungu katika umbo la Roho, wewe ukiwa na Neno Lake ndani yako, hapo Yeye anaingia ndani. Kama ukipokea Neno ndani yako, Roho Mtakatifu ndicho kitu pekee ambacho kinaweza kufanya hilo liishi, ndipo basi unapata ahadi ya kumiliki mlango wa kila adui anayejaribu kukushambulia. Hiyo ni kweli. Mungu aliahidi hilo, na ndivyo ilivyo.

29 Sasa, kumbuka, unaweza tu kulifanya hilo hapo, na hapo tu, baada ya kujaribiwa kwa Neno.

30 Ibrahimu alijaribiwa kwa Neno. "Je! utaamini, Ibrahimu, kwamba utapata mwana?"

"Ndiyo."

31 Mwana akaja. "Sasa mwangamize. Je! bado unaamini hilo, Ibrahimu?"

32 "Ninaliamini, hata sasa, kwani Wewe waweza kumfufua katika wafu."

33 Na baada ya hayo, Yeye akasema, "Sasa, Uzao wako utamiliki lango la adui wake." Amina! Baada ya jaribio kuja!

34 Hebu na tuchunguze baadhi ya Uzao wa Ibrahimu, katika uzao wa asili. Jambo ambalo, sisi leo hii ndio Uzao wa kiroho. Lakini hebu na tuone, kwa uzao wa asili, habari za baadhi yao ambao waliamini ahadi yote, ya Mungu, na hawakuswa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

35 Nilisema, tena, "Kwa nini msichana wa Kikristo aonyeshe rinda lake la ndani? Siwezi kuelewa hilo."

36 Umezaliwa mara ya pili, na Mungu, unao uzuri wa Roho Mtakatifu kuonyesha kile ulicho wewe, ndicho ulicho. Unao wema ambao hizi rinda za aibu hazina. Hilo ni kweli. Mwanamke halisi wa Mungu, ambaye husimama na wema,

unaweza uchekwe, na kuitwa mtindo wa zamani, lakini una kitu ambacho hawawezi kugusa, na wamekwisha kukipoteza na kamwe hawawezi kukipata tena. Hilo ni kweli. Mna wema. Hicho ndicho Mungu anachoangalia, ni wema. Mnaona?

37 Lakini jambo la kwanza, kama kuna swali moyoni mwako, usilitende kamwe. Usije kwenye mstari wa maombi kama kuna swali moyoni mwako. Usije isipokuwa unaliamini yakini, kwa mkazo, hakuna wimbi lo lote moyoni mwako, kabisa, ila kwamba utaponywa, hapo utaondoka jukwaani hapa mtu mzima. Hiyo ni kweli, kunapokuwa hakuna swali moyoni mwako, kabisa. Lazima umwamini Mungu, si kujifanya unaamini. Uamini kwelikweli!

38 Na Uzao wa Ibrahimu unaamini hilo kwa sababu Neno limesema hivyo, na hiyo ndiyo sababu tunaliamini. Sio kwa sababu mtu fulani ametoa makosa, kwa sababu mtu mwingine alisema hivyo. Kwa sababu Mungu alisema hivyo, hilo linalifanya kuwa Kweli. Mungu anapolinena, hilo latosheleza maswali yote. Yeye ndiye Neno la mwisho. Ndiye uamuzi wa mwisho. Mungu anaposema jambo lo lote, hilo latosha. Hakuna kitu kingine cho chote kiwezacho kunena dhidi yake. "Kila neno la mwanadamu liwe uwongo, na Langu liwe Kweli."

39 Sasa tunapowachunguza baadhi ya wazao hawa, hebu tufikirini. Tunawafikiria wale watoto wa Kiebrania, ninao hapa, tunapowazia hilo, juu ya wale watoto wa Kiebrania, baada ya kujaribiwa dhidi ya ibada ya sanamu. Sasa, mnakumbuka, mfalme alisema, "Ye yote ambaye hatasujudia sanamu hii, atatupwa katika tanuru ya moto." Sasa, watoto hawa waliamini kwamba Neno la Mungu ni kweli, kwamba hawapaswi kuabudu sanamu ya namna yo yote, lakini walipofika kwenye shindano la kuamua walijaribiwa kama wangeabudu.

40 Wakati, watoto wengine wote chini kule walitii na wakaenda kuabudu, waliambatana na alilosema mfalme. Waliambatana na wazo lililopendwa na watu wa zamani hizo, kwamba lazima watende hilo.

41 Nao walipojaribiwa, kama wangeabudu sanamu na kuvunja Neno la Mungu, walidumu waaminifu kwa Neno. Bila kujali hali zilivyo, walidumu waaminifu kwa Neno. Nao walipowatupa kwenye tanuru ya moto, ahadi ya Mungu ilitimizwa. Walimiliki malango ya adui zao. Na palikuwa na Mtu wa nne amesimama mle ndani, akiwa na ufunguo uliotoa joto katika moto ule, na haukuweza kufanya lo lote ila kuwaweka huru. Amina.

42 Wakati mwanamume au mwanamke yuko tayari kupata jaribio, jaribio la kuhakikisha kabisa!

43 Unaona, iliwabidi waende motoni. Na basi walipoenda, walikuwa motoni, na jambo pekee lililotukia, hili jaribio la moto lilifungua tu, liliondoa zile—zile kamba kwenye mikono yao.

44 Mara nyingi, Mungu hutuachilia, wakati tunapofungwa kabisa na ulimwengu, tumefungwa, Yeye huruhusu majaribu makali yatujie, ambapo inatulazimu kufanya uamuzi. Na tunapofanya hivyo, jambo pekee lile jaribu liwezalo kufanya, wakati Mzao halisi wa Ibrahimu anasimama kwenye njia—njia panda ya uamuzi, naye anafanya uamuzi wake kumtumikia Mungu, inaweza tu kukata zile kamba na kutufanya huru. Shetani anaweza akupe ugonjwa. Anaweza akupe jambo moja, jingine. Wajuaje siye Mungu aliyekuweka kwenye njia panda, kuona u—utafanya uamuzi wa jinsi gani?

45 Walimiliki lango la ule moto. Moto haukuweza kuwaunguza. Hata hapakuwa na harufu ya moto juu yao, kwa sababu walijua kwamba wao ni Uzao wa Ibrahimu, nao walisimama upande wa Mungu na Neno Lake. Walimiliki yale ma—malongo ya adui, na ule moto haukuweza kuwachoma, kwa sababu walimiliki malango.

46 Baadaye, palitokea mtu, nabii chini huko, jina lake Danieli. Alijaribiwa kama angemtumikia Mungu mmoja wa kweli, au la. Na ilipofikia wakati ule, kama angemtumikia Mungu mmoja wa kweli au kumwabudu mungu wa kishenzi, yeye alikataa kufanya hivyo; akateremsha mapazia, na kuomba kwa Mungu wake, kila siku. Naye alihukumiwa kwa ajili ya hilo, kwa adhabu ya sheria za serikali kuu, kisha alitupwa katika tundu la simba. Kundi la simba wenye njaa walimngurumia. Alifanya nini? Alimiliki lango la adui wake. Simba hawakuweza kumla. Mungu alishusha chini Nguzo ya Moto, Malaika aliyesimama kati yake na simba.

47 Alimiliki lango la adui, kwa sababu alijaribiwa kuona kama angemwabudu Mungu mmoja wa kweli, au awe na miungu dazeni moja ya kishenzi ambayo aliabudu. Kwa hiyo alistahimili lile jaribio, naye akamiliki lango la adui. Simba hata hakuweza kumgusa, kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye. Ahadi ya Mungu ilidumu kweli, kwani alikuwa Mzao wa kweli wa Ibrahimu.

48 Musa, loo, mwingine maarufu. Alijaribiwa, pia, kuona ahadi ambayo Mungu alimpa. "Nitakuwa pamoja nawe ushukapo kwenda huko." Naye aliposimama mbele ya waigizaji wa kipawa chake, Yane na Yambre walijaribu kusimama na kuigiza kitu kile hasa ambacho Musa aliamriwa kutenda. Naye Mungu alikuwa amemwita, naye alijua ndiye ambaye ameagizwa kufanya jambo hili, naye akasimama pale na kutenda ule muujiza kama Mungu alivyomwambia kutenda. Na hapa walisimama waigizaji, kufanya jambo lile lile, lakini halikumhangaisha Musa. Alisimama mwaminifu kwa Neno la Mungu, naye akamiliki malango, amina, ya adui, kwa sababu alisimama mwaminifu kwa ahadi ya Mungu, haidhuru nani alijaribu kuliigiza.

49 Ni somo jinsi gani kwa kila Mkristo! Unapoangalia kila upande na kuona mnafiki, basi kumbuka tu yeye anajaribu kuigiza kitu cha kweli. Lakini, hilo linamaanisha tu kuna mmoja ambaye ni wa kweli. Simama mwaminifu kwa Neno la Mungu! Haidhuru kuje nini au kwende nini, shikilia ahadi Yake. Ndiyo, Danieli alidumu mwaminifu kwa Neno la Mungu.

50 Haidhuru wangapi walijaribu kumwigiza, na kila kitu, alidumu mwaminifu. Naye alikuja kwa kusudi fulani, kuwatoa Israeli kutoka Misri, na kuwapeleka katika nchi ya ahadi. Na wakati wao ulipotimia wa kuingia nchi ya ahadi, kutoka Misri, Bahari ya Chumvi imesimama njiani. Naye akamiliki malango ya maji, mara malango yakafunguka. Na yale—yale maji yakarudi nyuma, ndipo Musa aliwapeleka Israeli hadi nyikani, kwenye mlima ambao Mungu alimwagizia awalete. Amina. Yeye akamiliki malango ya adui.

51 Baba yake, Ibrahimu, alikuwa na ahadi ile, kwamba Uzao wake wa kweli ungemiliki lango la adui. Na malango ya maji yalifunga, naye hakuweza kupita, nayo hiyo ilikuwa njiani mwake akiwa kazini. Alitakiwa kuwaleta watoto wale kwenye mlima ule. Mungu alimwambia awalete. Na hapo likasimama lango njiani, naye akamiliki lango la adui.

52 Yoshua, baada ya kitambo kidogo, walipokuja Kadesh-barnea, ambapo palikuwa kiti cha hukumu cha ulimwengu wakati ule, hapo Israeli akafikia hukumu yake. Tunamwona Yoshua pamoja na Kalebu, na wengine kumi na wawili . . . au—au wengine kumi. Mmoja toka katika kila kabila alitumwa kule kuipeleleza nchi waliyokuwa tayari kuipokea.

53 Nao walipoona hayo majitu makubwa yamesimama pale, kumi kati yao walijisikia vibaya sana, wakasema, "Hatuwezi kuichukua. Ni kubwa mno. Mbona, angalia upinzani tulio nao." Lakini waliporudi kuleta taarifa, walileta ripoti mbaya.

54 Kwa nini wangeleta ripoti mbaya, iwapo Mungu aliwaambia, "Nimewapa ninyi nchi ile; ni yenu"? Yeye aliwaambia chini huko Misri. "Nimewapa nchi hii. Ni nchi nzuri. Imejaa maziwa na asali."

55 Bali walipoona kwamba ule upinzani ni mkuu mno, kumi kati yao wakarudi na kusema, "Hatuwezi kulitenda."

56 Ilikuwa Yoshua, aliyewatuliza watu, akasema, "Twaweza kuimiliki bila shaka. Tunaweza bila shaka!" Kwa nini? Alikuwa akiangalia ile ahadi. Alikuwa Mzao wa kweli wa Ibrahimu. Haidhuru upinzani ulikuwa namna gani, "Twaweza kumiliki hilo lango, kwa sababu Mungu aliahidi nchi." Naye akamiliki lango.

57 Baadaye, alipowaleta wana wa Israeli pale mtoni. Huo hapo, katika mwezi wa Aprili, ule mto mkuu, ukifurika. Yordani ukitiririka toka milimani, nao umeenea kote uwandani. Ilionekana kana kwamba ndiyo majira mabaya zaidi, mwakani,

ambapo angeliweza kuwa kule. Bali, hata hivyo, alikuwa mzao wa Ibrahimu. Alijua alikuwa na ahadi, naye alikuwa kazini. Mungu alimpa ono, jinsi ya kulitenda, naye akamiliki malango ya ule mto. Mara yale malango yalipofunguka, maji yalirudi hadi milimani. Ndipo Yoshua na Israeli wakamiliki malango ya adui, na kuvuka hadi nchi ya ahadi, kwa sababu Mungu aliwaambia wafanye hivyo. Uzao wa kweli wa Ibrahimu!

58 Ndugu na dada, alipofika kule, Yeriko wote ulizungushiwa ukuta, juu vya kutosha hata wangeweza kuendesha magari matatu juu yake. Waisraeli hawa wangewezaje kutenda hili huku wana panga walizoazima, na zingine wakaokota, na kila ghasia, na fimbo na mawe, wangewezaje kuingia humo? Lakini bado yeye alikuwa Mzao wa Ibrahimu. Mungu alimpa ono, akamwambia jinsi ya kulitenda, kasema, "Pigeni tarumbeta." Amina. Ndivyo. "Pigeni kelele, pigeni hatua taratibu kuelekea kwenye ukuta, malango yataanguka mbele zenu." Amina! Alikuwa Mzao mwaminifu wa Ibrahimu. Alikuwa mwamini halisi wa Mungu. "Malango yataanguka chini mbele yenu. Pigeni tu kelele, na mpige baragumu. Hilo tu ndilo liwapasalo kutenda." Basi kulitukia nini? Malango yalianguka chini, na Yoshua akauteka ule mji.

59 Baadaye kidogo, tunaona kwamba adui alikuwa anawavamia na kuendelea, baada ya hayo, na hata Yeye akasimamisha jua papo hapo. Kama nilivyozungumza asubuhi hivi majuzi, juu ya *Kitendawili,* Yeye alisimamisha jua mpaka akamiliki malango ya adui wake. Amina. Alijua kwamba huyo adui akiwahi kukusanyika pamoja tena, walikuwa wametawanyika, na jua lilikuwa linatua, na Waamori na Waamaleki, na kadhalika, walikuwa wametawanyika kabisa. Wakija tena, kisha wakusanyike, basi angekuwa na wakati mgumu kuwapiga akawafukuza tena. Na kulikuwa na kitu kimoja tu ambacho kilikuwa kinashikilia, nacho kilikuwa ni wakati. Basi Yeye alisimamisha wakati. Amina! Amina! Kuna kitu kimoja kinachomzuia kuifikia ile ahadi, nacho ni jua, maumbile yenyewe yakimzuia apite, ndipo Yeye akakomesha maumbile. Kwa nini? Alikuwa Mzao wa Ibrahimu. Aliamini ahadi ya Mungu. Alimsimamisha, akayamiliki malango hayo. Ndiyo, bwana.

60 Watu hawa mashuhuri, wote ni watu mashuhuri. Lakini unajua wakati wao, kila mmoja wao, walipofika kwenye lango la mauti, wote walikufa. Kila mmoja wao ilibidi afe. Kwa sababu walikuwa watu mashuhuri, "Walifumba vi—vinywa vya simba, na wakaepuka moto, na makali ya upanga," na kadhalika, kama tunavyoambiwa katika Waebrania 11. Nao wakamiliki malango ya adui, wote isipokuwa adui mmoja, naye huyo ni mauti. Mauti yalimmeza kila mmoja wao.

61 Kisha siku moja, akaja Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu; Mzao wa Ibrahimu, kwa imani. Si

kwa Isaka, uzao wa asili; hao walitenda sehemu yao. Lakini hapa yuaja Mtu Ambaye hakuzaliwa kiasili. Hapa yuaja Mtu ambaye kamwe hakuja kwa tamaa ya kimwili. Hapa yuaja Mtu kwa uzazi wa kibikira. Mwana wa Mungu, Mzao wa Ibrahimu, jinsi huyu alivyokuwa Mtu mkuu! Wengine wa kiasili walizaliwa kwa uzazi wa kiasili. Mtu huyu alizaliwa kwa uzazi wa kibikira. Alifanya nini alipokuja duniani? Alishinda kila adui aliyekuwa naye Shetani. Alishinda kila kitu.

62 Alifanya nini? Alienda Zake akashinda maradhi. Hakungeweza kuwa na maradhi karibu Yake; kila mahali yalipokuwa na maradhi, Yeye aliyashinda. Alifanya nini baada ya kuyashinda? Alitupa sisi funguo, amina, akisema, "Cho chote mtakachofunga duniani, nitakifunga Mbinguni." Loo! Amina! Huo ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ahadi Yake. Roho Mtakatifu ndani yetu sasa, tukiwa na funguo, tukizielekeza kwenye maradhi. Yeye alishinda maradhi. Maradhi hayawezi kusimama Mbele Zake. Na Yeye alisema kwamba ametupa funguo kutenda jambo lilo hilo, kushinda maradhi. "Lo lote mnalofunga duniani, Mimi nitalifunga Mbinguni."

63 Pia, majaribu, Yeye alijaribiwa kwa kila namna kama sisi. Alifanya nini? Yeye aliyashinda. Naye alituambia nini? "Mpingeni shetani, naye atawakimbia." Yeye alishinda maradhi kwa ajili yetu. Akashinda majaribu kwa ajili yetu, akavunja malango; akamnyang'anya ibilisi funguo, na kuzikabidhi mwamini, wa Uzao wa Ibrahimu, na kusema, "Kama akiwajaribu, mpingeni, naye atawakimbieni." Loo, jamani! Mpingeni!

64 Yeye alishinda mauti na kuzimu pia. Yeye alifufuka siku ya tatu, akisema, "Nimeshinda. Na kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai." Loo, ni ahadi jinsi gani! Hiyo ni kwa Mzao wa Ibrahimu. Yeye alishinda kaburi, akafufuka siku ya tatu, ili tupate kuhesabiwa haki. Yeye alipofufuka, alikuwa kuhesabiwa haki kwetu. Hilo latufanya sisi nini? Alishinda maradhi. Alishinda mauti. Yeye alishinda kuzimu. Alishinda kaburi. Alishinda majaribu. Loo!

65 "Sasa tu zaidi ya washindi kwa Yeye aliyetupenda na kuutoa uhai Wake kwa ajili yetu," akiwa Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Tukiwa na Roho yule yule wa Mungu ndani yetu, ambaye alikuwa ndani Yake, tu zaidi ya washindi. Kila lango limekwisha kushindwa kwa ajili yetu. Jambo pekee litupasalo kufanya ni kulimiliki. Limekwisha kushindwa. Maradhi yameshindwa. Kifo kimeshindwa. Kuzimu kumeshindwa. Kaburi limeshindwa. Kila kitu kimeshindwa, nasi tunashikilia funguo, kwa neema Yake. Unaogopa kuzitia kwenye kufuli, na kusema, "Naja katika Jina la Yesu Kristo."? "Muombeni Baba lo lote katika Jina Langu." Nampenda.

66 Baada ya miaka elfu mbili kupita, miaka elfu mbili, na bado Yeye yupo hapa miongoni mwetu, yule Mshindi mwenye nguvu nyingi ambaye alipasua lile pazia vipande viwili, ambaye aliondoa kila maradhi, kila ugonjwa, akajitweka kila kitu, Mwenyewe, kisha akachukua udhaifu wetu mpaka msalabani, na maradhi yetu na magonjwa yetu, akavishinda, naye akafufuka ili tupate kuhesabiwa haki, naye yu hai baada ya miaka elfu mbili, kujidhihirisha Mwenyewe kama Yesu Kristo aliye hai, miongoni mwa Uzao wa kifalme wa Ibrahimu ambao ni warithi wa mambo yote. Loo, jamani! Wale ambao baadaye, hupitia jaribio lile, ahadi ya Neno! Kama unaweza kuamini Neno, basi wewe pia u Mzao wa Ibrahimu. Hivyo ndivyo unavyofikia jambo Hilo.

67 Kama huwezi kustahimili jaribio la Neno, basi kama unalitilia Hilo shaka, shaka kidogo, ni vigumu kwako kuamini Hilo, kuna jambo fulani au jingine, huwezi kuamini Hilo, basi usije kwenye mstari wa maombi. Hata nisingejipumbaza madhabahuni, mpaka uweze kupata neema ya kutosha kujua kwamba Neno la Mungu ni kweli.

68 Na mara unapovunja pazia hilo la kutokuamini, basi unazo funguo mikononi mwako, za mauti, kuzimu, na kaburi, kwa sababu unaye Mshindi Ambaye alishinda kwa ajili yako. Ndipo una Waebrania 13:8, ambayo inatuambia, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Twawezaje kulitenda?

69 Watu leo husema, "Loo, vema, nitakuambia, Yeye Ndiye kwa—kwa namna fulani, Yeye Ndiye."

"Ni yeye yule," Biblia ilisema.

"Loo, vema, Yeye hatendi leo hii kama alivyotenda."

70 Tunaliona sasa hivi, tunapoona Neno Lake likithibitishwa. Inafanya nini? Inalitupa Hilo moja kwa moja katika mapaja yao tena. Amina.

71 Uzao halisi wa Ibarahimu unaliani. Wanalijua. Naye anasimama, usiku wa leo, kama alivyokutana na Ibrahimu juu kule katika siku za Lutu na akafanya muujiza ule, kama alivyofanya kwa kumwambia Sara kile alichosema nyuma Yake. Yesu aliahidi, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, kwamba Kanisa lingeona jambo lile lile kabla tu ya Kuja Kwake. Ni nini? Lazima litukie. Mungu aliliahidi. Yesu Kristo alilithibitisha na kusema lingekuwa hivyo, na sisi hapa leo, baada ya miaka elfu mbili, twamuona Yeye miongoni mwetu, bado yungali Mshindi mwenye nguvu! Yeye alishinda mauti, kuzimu, kaburi, ushirikina wote; akachukua Neno . . .?. . . yeye. Ndiyo.

72 Yeye alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtapewa." Ilikuwa nini? Neno, Kristo, Ambaye yuko moyoni mwako. "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi mmeshinda kila kitu sababu nimeshinda kwa ajili yenu. Mkikaa ndani

Yangu, kama mnaweza kunielewa Mimi, kama mnaweza kukaa ndani Yangu. Yeye aniaminiye Mimi, yeye anipokeaye Mimi; siyo kujizingizia, lakini awezaye kupokea. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, anayeelewa Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; na hataingia katika majaribu, au hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani." Huyo hapo, yule Mshindi mwenye nguvu!

73 Huyu hapa leo hii, yeye yule jana, leo, na hata milele. Huyu hapa akitenda mbele ya Uzao wa Ibrahimu, ambao wameitwa kutoka Babeli, wameitwa toka Sodoma, wameitwa kutoka ulimwenguni, na kutengwa, akionyesha ahadi Yake sawa kabisa. Baada ya miaka elfu mbili, Huyu hapa amesimama miongomi mwetu, usiku wa leo, yule Mshindi mwenye nguvu, Neno la Mungu Ambaye anaweza kutambua mawazo yaliyo ndani ya mioyo, na makusudio yake. Ni kitu gani? "Uzao wako utamiliki malango ya adui wake." Ni kitu gani? Ni Uzao wa Ibrahimu, Uzao wa kifalme, wakiamini Neno. Na Neno ni—Neno ni Mungu.

74 Sasa tuonapo hili, twaweza kupaza sauti pamoja nao, kama yule mshairi wa zamami.

> Maishani, alinipenda; kifoni, akaniokoa;
> Alipozikwa, aliondolea mbali dhambi zangu,
> Alipofufuka, akanihesabia haki milele;
> Siku moja Yeye yuaja, Lo siku yenye
> utukufu!

75 Mtu fulani alisema, "Unazeeka, kijana." Siwezi kulizuia hilo.

76 Nimeishi tangu nikiwa mvulana mdogo, tendo langu la pekee nililopata kufikiliza ni kuona Kuja kwa Yesu Kristo. Nimetoa maisha yangu kwa kusudi hilo. Bado niko mimbarani, kama mzee, ninaamini Hadithi ile ile, na jambo kuu zaidi ya yote niwezalo kufikiria ni kumwona Yesu Kristo akija kutoka mbinguni kupokea walio Wake. Mungu, basi . . . Si ajabu twaweza kuimba.

> Nyote lisifuni Jina la Yesu,
> Malaika na wamsujudie;
> Ileteni taji ya kifalme,
> Mkamvike taji awe Bwana wa wote.

77 Kwa nini? Yeye ni Mshindi mwenye nguvu nyingi. Kama wewe uko ndani Yake, uko katika Neno. Yeye alisema, "Kama mkikaa ndani Yangu, ombeni lote mtakalo." "Lo lote mtakalo," kwa maana kila lango limekwisha kushindwa. Basi tunaweza kusema:

> Kwani kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu,
> Kila sura, kila aya, na mstari;
> Ninatumainia Neno Lake la Kiungu,
> Kwani kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu.

78 Rafiki, hivi mnatambua hilo linamaanisha nini? Kila ahadi ambayo Mungu alimfanyia Ibrahimu, kila ahadi iliyonenwa na manabii, kila ahadi ambayo Yesu Kristo aliahidi kwa siku hii, Yeye yupo hapa kuthibitisha na kuonyesha kwamba Yeye yu hai milele. "Uzao wako utamiliki lango la adui."

79 Ifikapo saa ya kifo. Unasema, "Vipi kuhusu hiyo?" Bado una Milki ile ambayo Paulo alisema. "Ewe kaburi, ku wapi kushinda kwako? Ee mauti, u wapi uchungu wako? Lakini Mungu ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Mshindi yule mwenye nguvu nyingi, Yesu Kristo." Loo!

Malaika na wamsujudie;
Ileteni taji ya kifalme,
Mkamvike taji awe Bwana wa wote.

80 Usiku wa leo, baada ya miaka elfu mbili, twasimama kumuona Yeye, yuangali, yule Mshindi mwenye nguvu nyingi, Ambaye alipasua pazia ambalo lilitutenga sisi na ahadi yo yote ya Mungu, nasi tu zaidi ya washindi katika Yeye.

Hebu na tuombe.

81 Baba wa Mbinguni, tusimamapo hapa, usiku wa leo, katika Uwepo wa Roho Mtakatifu, Utu ule mkuu wa Yesu Kristo katika umbo la Roho, Ambaye aliahidiwa kuja juu ya Uzao wa Ibrahimu, Mzao wa kifalme. Twaomba, Ee Mungu, kama kuna mwanamume au mwanamke, mvulana au msichana, ndani humu, ambaye hakujui Wewe; wana shaka na machafuko niani mwao, kuhusu Neno la Mungu, ama ni Kweli ama la. Ee Mungu Mkuu, uliyeitoa hiyo ahadi, njoo usiku wa leo! Kuna ahadi moja kuu uliyoitoa, Bwana; Wewe waweza kuifikiliza ahadi ile, Wewe ulisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Baba, Mungu, tunaomba kwamba Wewe utathibitisha Neno Lako.

82 Wapo wengi wa watoto wa Ibrahimu hapa usiku wa leo, ambao ni wagonjwa. Loo, ibilisi amewafungia; wamewatia ndani, na wamepindua ufunguo, na kusema, "Sasa lazima ufe; una matatizo ya moyo. Una *hili, lile,* au *jingine,* na lazima ufe."

83 Ee Mungu, hebu ile tarumbeta ya sikukuu ilie, usiku wa leo, ya Injili, kwambahuru! mtumwa awe huru! Yesu Kristo ameshinda malango yale. Tunashikilia zile funguo mikononi mwetu. Loo! "Kwa Jina Langu watatoa pepo. Kama mkimuomba Baba lo lote katika Jina Langu, nitalifanya. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi Yeye naye atazifanya. Neno la Mungu ni kali na lina nguvu zaidi kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, ukikata na kugawanya mafuta yaliyomo, na hata huyatambua mawazo yaliyo katika moyo."

84 "Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, kwani walikuwa wakila, wakinywa, wakioa na kuolewa; mipango

mikubwa ya ujenzi." Nasi twauangalia ulimwengu. "Kutakuwa na ishara, mambo ya kutisha mbinguni juu (hii ni visahani vinavyoruka), matetemeko ya ardhi mahali mahali, bahari ikivuma (mawimbi ya bahari), watu wakivunjika mioyo (hofu), dhiki ya mataifa, wakifadhaishwa na wakati huo."

85 "Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Ee Mungu, njoo usiku huu ukatekeleze Neno Lako, njoo usiku wa leo na utakabali imani ya watoto wa Ibrahimu. Kwa Jina la Yesu Kristo twaliomba. Amina.

86 Bwana awabariki, sana. Sitatoa wito wa madhabahuni wakati huu. Nitawaacheni mjiamulie wenyewe. Nafikiri kwamba, mara nyingi, miito ya madhabahuni . . . Naamini pamoja nao. "Lakini wote waliopokea, walibatizwa." Naam, ni hivyo, "Wengi waliompokea Yeye." Tutawaombea wagonjwa.

87 Ningeweza kuzungumza hapa usiku kucha. Mu wasikilizaji wazuri. Bali ninalosema ni binadamu tu; bali kama nasema Maneno Yake, basi siyo maneno yangu, ni Maneno Yake. Kama nikisema kitu fulani, na Mungu hakitekelezi, basi hilo lilikuwa ni neno langu. Kama nikisema Neno Lake, na Yeye alitekeleze, ni nani yule mwanamume mwenye dhambi au mwanamke, mvulana au msichana, ambaye ataenda zake na kusema sivyo lilivyo?

88 Yesu, alisema wakati Yeye alipotenda mambo haya, wao walisema, "Mtu huyu ni mpiga ramli. Yeye ni pepo!" Mpiga ramli, mtu ye yote anajua kwamba kupiga ramli ni jambo la ibilisi. Yeye alisema, "Yeye ni mpiga ramli." Lakini uliwahi kuona mpiga ramli akiihubiri Injili? Uliwahi kumuona mpiga ramli akitoa pepo? La, hasha, hawafanyi hivyo.

89 Yeye alisema, "Sasa, Mimi Mwana wa Adamu nitawasamehe jambo hili. Bali Roho Mtakatifu ajapo, kunena dhidi Yake halitasamehewa katika ulimwengu huu au ulimwengu ujao, kwa sababu ni kuita kazi ya Mungu roho mchafu."

90 Mungu uturehemu, usiku wa leo, nami maomba kwamba Mungu atashuka na kuthibitisha Neno hili mbele yenu.

91 Ndugu, dada, hii ni nafsi yangu. Sina budi nikutane na Mungu. Ninawajibika kwa kile ninachowaambia. Mungu atalitaka kwangu. Hilo ni kweli. Itanifaa nini kusimama hapa na kusema mambo haya kama nimejua ninaihukumu nafsi yangu iende kuzimuni?

92 "Ipo njia ambayo inaonekana kuwa sahihi machoni pa mtu, bali mwisho wake ni njia za mauti." Mungu hahitaji mfasiri. Kama nilivyosema, Yeye hujifasiria Neno Lake.

93 "Uzao wa Ibrahimu utamiliki lango la adui." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

94 Kama ningeweza kukuponya, ningelitenda. Kristo amekwisha kukuponya. Kitu pekee, unazo funguo mkononi mwako. Ufunguo huo ni imani yako, kuishikilia. Lifungue, usiku wa leo, sivyo? Wakati Yeye anapokuja miongoni mwetu, Mshindi mwenye nguvu nyingi ambaye ameshinda kila ugonjwa, anakuja hapa na kuwaonyesha kwamba Yeye ametenda hilo, kwani Yeye bado ni Neno. "Na Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni."

95 Kadi gani ya maombi? B, moja hadi . . . Tungeanzia wapi, usiku wa juzijuzi? [Mtu fulani anasema, "Moja."—Mh.] Hebu tuanze na hamsini. Nani aliye na kadi ya maombi B, hamsini? Inua mkono wako juu. Kadi ya maombi B. Tulianzia toka moja, usiku wa juzijuzi, sasa tutaanzia toka hamsini, usiku wa leo.

96 Nani aliye na B, B, hamsini? Inua mkono wako. Kadi ya maombi B, hamsini. Mnamaanisha haipo hapa? Unayo? Sawa, B, hamsini. B, hamsini na moja, nani aliye nayo? B, hamsini na moja, sawa. B, hamsini na mbili, nani aliye na B, hamsini na mbili? Sawa, unayo. B, hamsini na tatu, hamsini na nne, njoo moja kwa moja hapa. Hamsini na nne, hamsini na tano.

97 Mwanangu hushuka anakuja humu, kabla tu sijaingia, na kuchanganya tita la kadi. Na mnaona jinsi zilivyo, moja *hapa* na moja *pale*? Hawajui. Waweza uje kwenye safu *hii* hapa na uchukue moja, wa pili achukue kumi, mwingine achukue ishirini na tano. Hatujui ipo wapi, bali, po pote zilipo.

98 Sasa, tungewaita wangapi? Watano, wanne? B, hamsini. Ilikuwa B, hamsini, sivyo? [Mtu fulani anasema, "Ndiyo."—Mh.] B, hamsini hadi hamsini na tano. Hamsini na sita, hamsini na saba, hamsini na nane, hamsini na kenda, sitini. Sasa hebu tuone, moja, mbili . . . Zihesabu, Billy, na tuta . . . Sitini, sabini, hebu na wasimame kwanza, tafadhali. B, hamsini hadi sabini, sabini na tano. Zihesabu, Ndugu Roy, tafadhali, wakati ninapozungumza na mkutano.

99 Ni wangapi nje huko sasa wakati mnapoangalia upande huu, nanyi hamna kadi ya maombi?

100 Kumbuka, Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Je, hilo ni kweli? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. Mnaamini hilo? ["Amina."] Uzao wa Ibrahimu ulisema hivyo.

101 Biblia inasema, kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu." Waebrania, sura ya 4, "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye angetenda hilo jinsi gani?

102 Kulikuwa na mwanamke mdogo, katika Biblia, kama mkiona ambalo ninazungumzia. Mwanamke mdogo, katika Biblia, pengine hakuwa na kadi ya maombi; bali alisema moyoni mwake, "Kama nikiweza kumgusa Mtu yule, ninamwamini Yeye." Alishatumia yote aliyokuwa nayo, kwa dak . . . na

madaktari. Hawakuweza kumsaidia. Hali yake ilikuwa mbaya mno. Hawakuweza kumsaidia. Bali aliamini kwamba Mungu angemsaidia. Naye akagusa upindo Wake, wa vazi Lake.

103 Naye alisema, "Naona kwamba nguvu zimenitoka." Sivyo?

104 Mnaamini Yeye ni yeye yule, usiku wa leo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Mnaamini Yeye yupo hapa? ["Amina."] Wangapi wanaamini Yeye amefufuka katika wafu? ["Amina."] Sasa unaweza kuthibitishaje Yeye amefufuka katika wafu?

105 Si muda mrefu uliopita, mtu mmoja maarufu Mbaptisti alikuja kwangu, naye akasema, "Ndugu Branham, nilishindwa—nilishindwa, wakati mmoja, na Mwislamu ambaye alisema hilo. Akasema, 'Kama Yeye amefufuka, Yeye aliahidi kwamba angetenda jambo lile lile. Hebu tumwone Yeye akilitenda.'" Unaona, wanaamini kwamba Yeye hakulitenda hilo.

106 Bali tunaamini kwamba Yeye analitenda. Tunaamini kwamba Yeye amefufuka katika wafu. Hakuwa dini nyingine ulimwenguni ambayo inaweza kuthibitisha kwamba mwanzilishi wao anaishi, isipokuwa Ukristo. Na njia ya pekee Mungu anaweza kulihakikisha Hilo, ni kwa wale ambao wanaliamini; kwani hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu hutekeleza Maneno Yake, ni wale ambao wanaliamini.

107 Sasa wakati wanapanga mstari huu mdogo wa maombi hapa. Sijui tutawapata wangapi. Nataka kila mmoja wenu, usitoke ulipo, usiondoke ulipoketi, usisogeesogee. Angalia huku na uombe, useme, "Bwana Yesu, ninaamini."

108 Mnakumbuka, Yeye aliniambia, "Kama ukiwafanya watu wakuamini; kisha uwe mwaminifu uombapo." Hilo limefanyika katika taifa hili lote, huku na huko, kwa miaka kumi na mitano, halijashindwa hata wakati mmoja. Haliwezi kushindwa.

109 Mungu, jambo moja Mungu hawezi kufanya, nalo ni kushindwa. Yambidi kuhifadhi Neno Lake. Mimi ninaamini hilo. Mimi ninaamini hilo kama tu vile mimi . . . kuliko ninavyoamini niko katika jengo hili; hii ingeweza kuwa mazigazi, huenda ikawa ni ndoto. Katika nafsi yangu, najua Yesu Kristo Mwana wa Mungu yu hai. Na wewe ukiwa Uzao wa Ibrahimu, wewe ukiwa umekufa katika Kristo, u Mzao wa Ibrahimu.

110 Sasa wana leso hapa. Mafanikio makuu yanapatikana kwa hawa, watu wanaoamini. Na tuinamishe sasa vichwa vyetu, wakati wanapojitayarisha, na kuombea hivi.

111 Baba wa Mbinguni, tunafundishwa katika Biblia, na pana watu hapa ambao wanaamini kila Neno ambalo Wewe umesema ni Kweli. Bwana, wakati mwingine wanasita na kugonga kwenye tundu la ufunguo, wanalikosea, na kulikwaruza, bali wanaamini lipo. Hebu na waendelee kugonga, wataliona, kwani lipo. Na ufunguo huo ni ufunguo wa kweli,

"Kama mkiweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Kama ule wimbo unavyoimbwa sasa hivi, au kuchezwa.

112 Katika Biblia inasema kwamba, "Paulo alichukua toka mwilini mwake leso na vitambaa, na wakavipelekea wagonjwa na walioteseka, na pepo wachafu wakawatoka watu, nao wakaponywa."

113 Sasa, Bwana, twajua Mtakatifu Paulo yu pamoja Nawe. Lakini, haikuwa yeye; ilikuwa Wewe, Bwana, Kristo ndani yake. "Si mimi ninayeishi, bali Kristo aishiye ndani yangu," yeye alisema.

114 Na sasa kwa kizazi hiki, bado Wewe ungali Kristo, leo hii, kama ulivyokuwa jana. Na ninapoombea leso hizi, nikizigusa, naomba kwamba Wewe utamshinda kila adui. Wape imani, kuwaacha wajue kwamba adui ameshindwa.

115 Na wakati mmoja, Bahari ya Shamu, kama tulivyozungumza habari zake sasa hivi, iliwatenga Israeli na ahadi, nao walikuwa kazini. Na mwandishi mmoja alisema, kwamba, "Mungu alichungulia chini kwa macho ya hasira, katika ile Nguzo ya Moto, nayo bahari ikafadhaika na kufungua malango yake, nao wakavuka."

116 Chungulia, usiku wa leo, katika Damu ya Yesu Kristo. Na jalia, leso hizi zikiwekelewa wagonjwa, hebu adui aone imani yetu, usiku wa leo, tunapoomba sala hii ya imani kwa ajili yake. Na jalia kila mmoja apone, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

117 Sasa nataka mnisikize kwa makini. Ye yote ambaye yupo kwenye maikrofoni juu hapa, waweza kuiongeza. Kwa sababu, kama Roho Mtakatifu angefanya hili . . . sisemi kwamba Yeye atafanya.

118 Sasa mtu ye yote akija hapa na kukuambia kwamba wana uwezo wa kuponya wagonjwa, usiamini hilo. Uwezo wote uko ndani ya Kristo. Yeye ndiye Mshindi, si wewe nami. Tunakubali tu ambacho Yeye ametenda. Hakuna mtu aliye na uwezo wa kuokoa au kuponya.

119 Kila mtu duniani, gharama imekwisha kulipwa tayari. Yaliyodaiwa yamekwisha kulipwa. Ilikuwaje? "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake tuliponywa." U—uponyo wako umekwisha lipiwa. Wokovu wako ulikwisha lipiwa. Unayo imani ya kuja, kulikubali? Ni hilo tu. Kama u Uzao wa Ibrahimu, unayo. Mungu aliliahidi. Kipo kitu ndani yako ambacho kinasema ipo, na ipo.

120 Sasa kipawa ni nini? Kipawa ni kuondoka kwenda kuwaponya watu? La. Kipawa ni kujiondoa wewe mwenyewe njiani, kusudi Mungu apate kukutumia.

121 Sasa Yeye aliahidi hiyo, ishara ya mwisho, kulingana na Yesu Kristo, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kabla tu haujateketezwa." Si kabla mambo mengine kutendeka, Injili

ilihubiriwa na Lutu, na kadhalika; si hiyo. Bali kabla tu haujateketezwa, Mungu alishuka katika umbo la binadamu, akaketi pamoja na Kanisa lililoteuliwa, Ibrahimu na kundi lake, ambaye alikwa na ahadi.

122 Sasa kumbuka, ni Uzao wa Ibrahimu tu unaopokea hili. "Kitambo kidogo na ulimwengu haunioni Mimi tena," Yesu alisema. "Ninyi mtaniona Mimi, kwani nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

123 Bali Yeye aliahidi, kabla tu ya kurudi tena, "Kama ilivyokuwa Sodoma," angalia Sodoma inapata nini; angalia Kanisa teule linalopata, kasema, "hivyo ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu." Mungu akidhihirishwa katika umbo la binadamu, huku mgongo Wake umeelekezwa hemani, alisema ambacho Sara alitenda mle ndani ya hema. Kila mtu anayejua hiyo ni Kweli, inueni mikono yenu. Hilo ni barabara kabisa. Sasa Yeye aliliahidi. Tuko katika wakati wa mwisho. Sasa kumbuka, hilo ndilo jambo la mwisho lililotukia; na ulimwengu wa Mataifa ukateketezwa, Sodoma, na yule mwana wa ahadi akatokea. Tunamtazama Mwana wa ahadi, Mwana wa Mungu.

124 Sisi hapa. Mungu na ayafungue macho yenu. Sijui kitu kingine cha kusema. Yeye na awafungue macho.

125 Sasa Baba wa Mbinguni, mimi ni mdhaifu vivyo hivyo, mimi ni fungu la udongo wa mfinyanzi ambalo umefinyanga pamoja, na kuliweka hapa. Ee Mungu, nijalie, usiku wa leo, nipe neema Yako na Uwepo Wako, ili kwamba upate kutumia madonge haya madogomagadogo ya udongo wa mfinyanzi uliyo nayo hapa. Kwamba wale, Bwana, ambao umewaita Wewe kwenye Uzima wa Milele, na labda bado hawajaukubali, wajalie waone ahadi hizi. Yawezekana wamefundishwa kwamba hiyo ilikuwa kwa siku nyingine, bali hili hapa katika Biblia. Lithibitishe, Bwana. Hiyo ni tafsiri Yako Mwenyewe. Haihitaji zaidi ya hilo. Kama utalifanya tu liwe hivyo, basi wataona kwamba Neno ni kweli. Tujalie, Bwana. Tunatoa nafsi zetu Kwako.

126 Mjalie kila mtu ndani hapa, Bwana, atumie imani yao, usiku wa leo. Hebu kila mtu wa Kabila la Ibrahimu, katika Yesu Kristo, apate imani, usiku wa leo, na akubali Uwepo Wako. Nasi tutakupa sifa. Amina.

127 Naam, hii ni ya mwi-. . .Sasa hili ni ajabu. Nawatakeni mnisaidie sasa, niombeeni. Kaeni kimya kabisa, msisogeesogee. Kaeni kimya, ombeni.

128 Sasa, unaona, ni kubadilisha toka uinjilisti, hata kujipumzisha mwenyewe hivi kwamba Roho wa Mungu anaweza kukuchukua kabisa katika kiwango kingine.

129 Sasa hapa amesimama huyu kijana. . .Sogea huku kidogo, bibi, na hilo ni sawa tu, ili nisiondoke kwenye hii maikrofoni. Unaona, sijui kitendekacho, unaona, na basi wakati mwingine,

wajua . . . Sasa njia pekee ninajua hili, ni—ni kwenye maikrofoni, unaona, na wanajaribu kulinasa kule, na sijui ni nini.

130 Sasa tu wageni mmoja kwa mwingine. Mimi sikujui, sijawahi kukuona katika maisha yangu. Lakini u kijana sana kuliko mimi. Na tulizaliwa labda umbali wa maili kadha kati yetu, na miaka mingi kati yetu. Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. Hilo ni kweli? Kama ni kweli, inua mkono wako juu ili watu waone. Naam, yeye ni mwanamke tu asimamaye hapa.

131 Angalia, tulirudishe kwenye Maandiko. Hebu tuchukue Yohana Mtakatifu 4. Kila mmoja wenu aisome mnapoenda nyumbani. Si—si kwamba mwanamke huyu ni mwanamke wa aina ile; sijui. Na unajua kwamba mimi si Yesu Kristo. Bali Yeye yupo hapa. Ni Yeye. Sasa Roho Wake akitutia upako, aweza kufunua shida yake, kama alivyotenda kwa yule mwanamke kisimani. Jambo lile lile.

132 Na, kwa hilo, ambapo makuhani na viongozi wa siku ile, walisema, "Mtu huyu ni mpiga ramli, au pepo, Beelzebuli."

133 Mwanamke huyu alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe u nabii. Twajua kwamba Masihi yuaja, na hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake."

134 Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, je! hiyo isingekuwa ndiyo ishara Yake usiku huu? ["Amina."] Je, Yeye aliahidi ingekuwa hivyo, kabla tu ya wakati wa mwisho? ["Amina."] Sasa angalia kama Yeye hutimiza ahadi Yake kwa Uzao wa Ibrahimu.

135 Sasa kama mtu ye yote ndani humu anafikiria hilo ni kosa, basi njoo hapa ufanye jambo lile lile. Kama sivyo, basi usiseme kitu kulihusu. Mmejaliwa.

136 Sasa, katika Jina la Kristo, naiweka kila roho chini ya mamlaka yangu, kwa utukufu na heshima ya Mungu.

137 Itanibidi tu nizungumze nawe kidogo, bibi mdogo. Unajua, Bwana wetu alizungumza na yule mwanamke kwenye kisima. Yeye alisema, "Nipe maji ninywe." Alikuwa anafanya nini?

138 Sasa angalia, Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5, "Amini, amini, ninawaambia, Mwana," huyo alikuwa ni Yeye, mwili, "siwezi kufanya neno lo lote Mimi Mwenyewe," ila lile alilomwona Baba akifanya. "Lile Baba afanyalo, Yeye humwonyesha Mwana. Unaona, siwezi kufanya cho chote Mimi Mwenyewe, isipokuwa nimemwona Baba akilifanya." Basi, Yesu kamwe hakutenda muujiza hata mmoja hadi kwanza Mungu amemwonyesha Yeye kwa ono; si kumwambia katika sikio Lake, bali alimwonyesha Yeye. "Ninaloona," si kusikia, "kumwona Baba akifanya." Hilo ndilo lililomfanya Yeye Nabii kama Musa, kama Musa alivyosema. Sasa wakati Yeye—Yeye alijua Baba . . . Yeye alikuwa katika . . .

139 Yeye alikuwa akienda Yeriko, bali alikuwa hana budi kupitia Samaria, basi akaja kwenye mji wa Sikari. Na sasa unaona, Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi.

140 Wayahudi walikuwa wakilitazamia hilo, Naye akawaonyesha ishara Yake. Filipo, Nathanieli, Petro, mara tu ishara ile ilipotendeka, walisema, "Wewe u Mwana wa Mungu."

Yule rabi alisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli."

141 Bali sasa kumbuka, Mataifa, sisi, tulikuwa Waanglo-Saxon, ha—hatukuwa tunamtazamia Masihi kamwe. Tulikuwa makafiri, Warumi, na kadhalika. Hatukuwa tukimtazamia Masihi kamwe. Yeye huja tu kwa wale ambao wanamtazamia Yeye.

142 Bali Wasamaria walikuwa wanamtazamia Yeye, kwa hiyo Yeye ilibidi apitie kwao, pande za juu karibu na Samaria. Yeye aliketi chini kisimani. Bibi kijana, labda karibu rika yako, alitokeza. Alikuwa mwanamke wa sifa mbaya. Umesoma hiyo hadithi, nadhani. Na Yeye akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

143 Akasema, "Loo, si kawaida kwa Wewe Myahudi, kumwomba Msamaria kitu kama hicho."

144 Yeye akasema, "Kama ungejua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji.'

145 Mazungumzo yakaendelea. Mwishoni, Yeye akaona shida yake ilikuwa wapi. Unakumbuka ilikuwa ni nini? Alikuwa na waume wengi mno. Kisha kasema, "Nenda kamlete mumeo, mje hapa."

Akasema, "Sina mume."

146 Akasema, "Umesema vema," akasema, "kwa sababu umekuwa nao watano, na yule unayeishi naye sasa si wako."

147 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe u nabii. Twajua yuaja Masihi, Yeye atatuambia mambo haya."

Naye akasema, "Mimi Ndiye."

148 Aliacha mtungi wake wa maji, akakimbilia mjini, akasema, "Njoni, muone Mtu Ambaye ameniambia niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hawakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Huyu hapa basi Mtu aliyedai kuwa Masihi, na akathibitisha kuwa na—nabii, na kuonyesha ishara ya Masihi.

149 Je, ingekufanya uamini kitu kile kile, kama Yeye alifanya jambo lile lile, kwa kuwa Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na ameahidi kwa Maandiko haya kwamba Yeye angelitenda?

Je, ingewafanya wasikilizaji waamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

150 Una maumivu ya figo. Kama hilo ni kweli, inua mkono wako juu.

151 Kwa nini hilo siku zote linaduta usoni mwangu? Mtu fulani asema, “Alibahatisha hilo.” Kamwe sikubahatisha hilo.

152 Hapa, yeye yu mwanamke mzuri. Je, unaniamini mimi? Sasa unajua kamwe sikubahatisha hilo. Hebu niseme jambo lingine. Mumeo yuko pamoja nawe. Yeye anaumwa, pia. Sivyo? Maumivi ya uti wa mgongo. Hilo ni kweli. Sivyo? Umekuja na mvulana mdogo. Anaumwa, pia. Unataka aombewe. Macho yake yana kasoro. Hilo ni kweli. Umekuja na msichana mdogo, ana shida ya figo, kama wewe. Hilo ni kweli? Sasa nyote mwaweza kuwa wazima, kama mtaamini. Mnaamini hilo? Mungu awabariki. Nendeni zenu mkaponywe.

153 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni nini? Yeye anajaribu kufanya nini? Kwenu ninyi, Uzao wa Ibrahimu, Yeye anawaonyesha kwamba hakufa. Siwezi kutenda mambo hayo. Yeye hajakufa. Bali yu hai, akiwaonyesha kwamba mnayo haki ya kumiliki malango ya adui wenu. Hilo latosha.

154 Ewe bibi, njoo huku, hebu kidogo. Sisi ni, kama wa rika moja, nafikiri. Bali tu—tu wageni mmoja kwa mwingine, kadiri nijuavyo. Sikujui, na sisi tu wageni. Sijui neno kukuhusu. Kama hilo ni kweli, inua mkono wako, unaona. [Yule dada anasema, “Hilo ni kweli.”—Mh.] Baadhi yao wamekupa kadi ya maombi, nawe huyu hapa. Sawa. Sasa kama Bwana Yesu . . .

155 Kama labda tuseme nilikuwa ninajaribu kuchukua mahali pa Ndugu Oral Roberts, au pa baadhi ya wale watu mashuhuri wa imani, ningesema, “Bibi, unaumwa nini?”

156 Ungesema, “Vema, nina *jambo fulani,”* na sasa yeye huenda asiwe sahihi. Unaona? Sijui. Unaona? Bali, yeye, unaweza umwambie anakoumwa.

157 Angekuwekelea mikono, aseme, “Mungu amenipeleka ku—kuombea wagonjwa. Unaamini hilo?” “Ndiyo.” “Mungu atukuzwe! Nenda, ukaamini hilo.”

158 Ni sawa. Ni sawa. Mungu aliahidi hilo. Bali, unaona, tunaishi juu zaidi kidogo katika si—siku kuliko hivyo. Yesu aliahidi, “Kama ilivyokuwa siku za Sodoma. Kazi nizifanyazo Mimi nanyi mtazifanya.”

159 Naam kama Mungu anaweza kuniambia jinsi ulivyokuwa, ungejua iwapo hilo ni kweli au la. Yeye aweza kukuambia utakavyokuwa. Na iwapo hilo ni kweli, hili litakuwa kweli, pia. Kama Yeye akikuambia, cho chote, sijui; lakini kama Yeye ataniambia shida yako ni nini.

160 Mtaamini, pia, enyi mkutano? [Kusanyiko, “Amina.”]

161 Kwa kweli yanipasa kukoma. Mara hiyo moja, mtu yule ambaye alikuwa hapa muda mfupi uliopita, hilo lapaswa kulithibitisha. Yesu alifanya hivyo wakati mmoja. Kamwe hakulifanya wakati mwingine tena. Kila mtu katika Sikari

aliamini, aliamini ushuhuda wa yule mwanamke, wakati alipokuja, akawaambia, naye alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya. Mkristo ameondoka jukwaani hivi punde tu; mbele zenu nyote! Amina. Lakini kwa kuwa muda umesonga zaidi kuliko tunavyofikiri, hebu Bwana na aendelee kujidhihirisha Mwenyewe, yule Mshindi mkuu, na mwenye nguvu nyingi, kusudi Uzao wa Ibrahimu. . .Bali kama Ibrahimu, Yeye alilitenda kwa ajili ya Ibrahimu, mara moja; kisha akauharibu huo, na akalifanya tena. Ibrahimu aliendelea kumwamini Mungu.

162 Haupo hapa kwa ajili yako mwenyewe. Upo hapa kwa ajili ya mtu mwingine, na huyo ni bibi. Ni dada yako. [Dada anasema, "Ee Bwana!"—Mh.] Na huyo bibi ana uvuli wa mauti. ["Jamani!"] Naye anaugua u—ugonjwa wa kisukari. ["Loo!"] Na yeye hatoki hapa. ["La."] Yeye anatokea . . . Anatoka Louisiana, nchi ya majimaji. ["Loo, loo, loo!"] Sawa. Na hapa pana jambo jingine, kusudi kusanyiko lipate kujua hili. Una binti ambaye ni mgojwa sana, ambaye anapanga kuhudhuria mkutano huu, naye ana kifafa. ["Loo, loo, loo!"] Hilo ni kweli. Hilo ni kweli. sivyo? ["Loo!"] Unaamini sasa? ["Ndiyo. Amina."] Kama wewe u Uzao wa Ibrahimu, likubali hilo na uende zako, ["Bwana Wangu! Bwana Wangu!"] na uponywe katika Jina la Yesu Kristo.

163 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Kumbuka, ni ahadi Yake. Yeye alisema angefanya hivyo. Yeye hutimiza ahadi Yake.

164 U hali gani? Tu wageni mmoja kwa mwingine. Sikujui. Bali Mungu anakujua. Unaamini kama Mungu anaweza kunifunulia shida yako, basi utajua lazima itoke kwa uwezo fulani wa kiroho. [Yule dada anasema, "Sawa."—Mh.] Sasa, kuna mambo mawili tu inaweza kutokea kwake, ambayo ungeweza kuwazia. Wakati inapotendeka, haiwezi kuelezeka kabisa, kwa sababu ni tukio la ajabu. Na, pia, ni kitendawili; jambo fulani, vema, halielezeki bali ni kweli. Ingekuwa kitendawili. Na sasa unalijua hilo, kama ni kweli au la, utajua kama Yeye amekuambia ukweli.

165 Sasa, kumbuka, mimi sikujui wewe. Lazima iwe ni Mtu fulani mbali na mimi. Kama ukitenda kama Mafarisayo, na kasema, "Loo, ni pepo mchafu," basi unapata dhawabu hiyo. Kama unaamini ni Kristo, unapata thawabu Yake. Sababu ya wewe kuweza kuliamini, ni kwa sababu Yeye aliliahidi kwa siku hii, na halijatokea tangu wakati ule hadi huu. Hilo linaufanya huu wakati wa mwisho.

166 Kuna mtu fulani anayeendelea kutokeza mbele yako, wakati wote. Ni mwanamume, ana mvi. Ni mumeo. [Dada yule anasema, "Ndiyo."—Mh.] Akiketi papo hapo. Anajaribu kukubali uponyo wake, akiwa ametiwa uvuli na kansa, ya uvimbe, kansa. Una shida ya figo, shida ya kibofu. ["Ndiyo."] Ninyi ni Bw. na Bibi.

Little. ["Ndivyo."]) Hilo ni kweli? ["Ndiyo."]) Aminini kwa mioyo yenu yote, nanyi mponywe.

167 "Unasema lake, majina yao? Mbona, bila shaka. Je! Yesu hakumwambia Petro, "Jina lako ni Simoni, mwana wa Yona?"

168 Hapa yupo mwanamume. Tu wageni mmoja kwa mwingine, bwana. Mimi sikujui wewe. Bali u mwanamume, kama—kama Petro akija kwa Bwana Yesu, tunakuja pamoja. Je, unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Unaamini nililokuambia ni kweli? [Yule ndugu anasema, "Ndiyo, bwana. Naamini, bwana."—Mh.] Kama unaweza kuliamini! ["Ndiyo, bwana."] Mimi, kama kuna cho chote ningeweza kukufanyia, ningekifanya, bali hakuna kitu ninachoweza kufanya. Yeye tayari amekwisha kifanya; ni kitu tu cha kukufanya wewe uamini. Basi, angalia, isingekuwa mimi. Kama ingekuwa ni mimi, ninge—ningekutendea yote niwezayo! Bali Yeye alinipa kipawa, nami hujiachilia mwenyewe mbele Yake, Naye anazungumza. ["Hilo ni kweli. Ndiyo, bwana."] Unaamini hilo? ["Ndiyo."]

169 Mnaamini hilo, mnaonisikiza? [Kusanyiko, "Amina."]

170 Nilitaka nimpate mtu. Una matatizo kadha. Bali moja ya mambo hayo ni, una uvimbe kwenye jicho lako la kulia. Hiyo ndiyo shida yako kuu. Hapa kuna jambo lingine, mwanamke anaendelea kutokeatokea hapa. Ni mkeo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mkeo hapa ana shida gani? Shida yake iko kinywani mwake. Ni meno yake. Hilo ni sawa. Unaamini kwamba Yesu yule yule, Ambaye aliyejua Simoni Petro alikuwa nani, angeweza kuniambia wewe u nani? [Yule ndugu anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ingekufanya uamini sana? ["Ndiyo, bwana."] Ungeamini? ["Ndiyo."] Oscar Barnes. ["Hiyo ni kweli."] Sivyo? Nenda zako nyumbani, ukaponywe.

171 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mgeni kwako. Mimi sikujui wewe, bali Mungu anakujua. Unaamini kwamba Yeye anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ungeamini hilo kwa moyo wako wote? Shida zako ziko kwenye sehemu za koo lako, na katika kifua chako hapa. Ni ku—kuoza kwa mfupa. Unapata marugurugu, vitu kama hivyo, na vifundo, ndani ya umbile la mfupa. Hilo ni kweli. Wewe hutoki hapa. Uko katika—katika mji uliozungukwa na miti ya machungwa kila mahali. Upo bondeni, na mandhari ya milima nyuma yake. Kuna hoteli iitwayo Antlers. Ni San Bernadino. Huko ndiko unakotoka. Rudi, Yesu Kristo akuponya, kama ukiamini hilo.

172 Kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuponya kansa, huyo ni Mungu. Je! unaamini Yeye atakuponya? [Yule ndugu anasema, "Hakika ninaamini."—Mh.] Amini hilo! Nenda zako na Bwana Mungu akufanye mzima kabisa kila mahali.

173 Sababu yako kuwa . . . kuwa na wasiwasi mno, umefadhaika sana. Kwa sababu ya wasiwasi hii, tumbo lako halina afya. Huwezi kuyeyusha chakula chako, kukileta kinywani mwako.

Ni kichungu sana kinywani mwako. Adhuhuri kuelekea jioni, unapata uchovu sana na kila kitu. Una kidonda tumboni mwako. Unaamini kwamba huyo ni Yesu Kristo awezaye kukuambia hilo? [Yule dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Nenda ule chakula chako cha usiku basi. Amini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo akuponya.

174 U hali gani? Kuna matatizo mengi. Bali moja ya mambo ambayo unayaogopa, utakuwa kiwete kwa yabisi kavu. Bali unaamini kwamba Mungu atakupa afya, akuponye hiyo? [Yule dada anasema, "Ndiyo."—Mh.]

175 Bwana Yesu, ninaomba kwamba Wewe utamkirimia dada yangu hilo. Mpe yeye—kuona kwake. Mwondolee bibi huyu hiyo shida ya mabibi aliyo nayo na umponye yabisi kavu, katika Jina la Yesu. Amina.

176 Enenda sasa, ukiamini. Yeye atalitenda, na hali itakuwa sawa. Usitie shaka, endelea tu kutembea, na uamini kwa moyo wako wote.

177 Shida ya ugonjwa wa moyo ni jambo la kutisha. Bali Kristo huponya moyo. Unaamini hilo? [Yule dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Nenda, amini hilo, nalo litatendeka, kabisa.

178 Unaamini utalemaa? La, sidhani, pia. Wazo langu, yabisi kavu; kivuli hicho hapo, loo, hiyo ni kansa. [Yule dada anasema. "Loo, loo!"—Mh.] Unaamini Yeye ataiponya? ["Ndiyo, naamini."] Nenda zako, liamini. Yeye atakufanya mzima.

179 Kumekuwa kukikusumbua, kukaacha kwa muda, kuziba kwa moyo. Bali unaamini kutakoma, usiku wa leo? Nenda zako, amini hilo, Yesu Kristo akufanya mzima.

180 Kumekuwa na shida dogo, kutokana na shida ya bibi, kwa muda mrefu. Na halafu, wewe, hupata shida sana kuamka asubuhi. Umekakamaa, katika viungo vyako. Unatembea kwa shida, mpaka wakati wa mchana, majira hayo. Ni yabisi kavu. Nenda zako, usitie shaka, hutakuwa nayo tena. Amini tu, kwa moyo wako wote.

181 Una mambo mengi, matatizo. Bali jambo moja ambalo linakukera sana, wewe pia unafikiria yabisi kavu, ambayo ndiyo, inakulemaza. Unaamini kwamba Yeye atakufanya utembee na akupe afya? [Yule dada anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Nenda, amini hilo kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya.

182 Moyo wenye wasiwasi, na yabisi kavu, bali unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima? Unaamini? Nenda zako, na Bwana Yesu akupe afya.

183 Tumbo hilo hakika limekupa shida nyingi sana kwenye miaka michance iliyopita, sivyo? Halitakutatiza tena. Nenda zako, amini hilo. Mungu akubariki.

184 Unaweza, pia, tumbo lako limepona. Nenda zako, amini kwa moyo wako wote. Usitie shaka.

185 Una wakati mgumu kupumua, pumu hiyo ya kale kweli inakuchosha. Sivyo? Unaamini itaondolewa sasa? [Yule ndugu anasema, "Ndiyo."—Mh.] Sawa, nenda ukaamini. Amina.

186 Halleluya! Mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

187 Hebu kidogo. Huoni ile Nuru pale? Bibi mmoja mweusi ananiangalia, ameketi papa hapa, ana uvimbe katika ubavu wake wa kushoto. Ana shida ya figo, matatizo. Ulikuwa na imani zaidi. Huhitaji kuja hapa. Umekwisha. Amini hilo tu. Amina. Uwe na imani kwa Mungu!

Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

188 Unaamini, dada, shida hiyo ya uti wa mgongo itakuondokea, unayeketi pale? Unaamini kwamba Yeye atakuponya? Sawa. Usitilie shaka, nawe waweza kulipata kama utaamini hilo tu.

189 Mwanamume aketiye hapa anayeniangalia, anaumwa na unyong'onyevu, kuamka usiku na kadhalika. Unaamini, bwana? Utakwisha, basi, kama ukiliamini.

190 Hapa ameketi mwanamume mweusi akiketi hapa, akiniangalia. Yeye anaugua kifafa. Yeye pia anatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Simama kwa miguu yako, bwana, ukubali uponyo wako. Mungu na akupe ubatizo wa Roho Mtakatifu. Amina.

191 Ng'ambo yako, kuna mtoto anayeketi kule, ambaye pia ana kifafa, kuzimia kwa mara kwa mara, ameketi kule, upande wa pili. Unaamini kwamba Mungu atampa huyo mtoto afya, hapo? Unaamini kwa moyo wako wote? Basi Mungu atamponya mtoto.

192 Mnaamini, kila mmoja wenu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Si—si Yeye, si Yeye kweli ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu? ["Amina."] Je, si Yeye ni yule Mshindi mkuu? ["Amina."] Si Yeye aliahidi ungeweza kumiliki malango ya adui? ["Amina."]

193 Ni wangapi wenu wamefungwa, wanasikia mgandamizo wa adui? Inueni mikono yenu, kwamba mnahisi mgandamizo wa adui. Nanyi ni Uzao wa Ibrahimu, inyosheni mikono yenu juu namna *hii.* Semeni, "Ndugu Branham, ninasumbuliwa na wasiwasi." Loo, kuna kama asili mia themanini kati yenu walio na hiyo. Aisee, mimi . . . Umekuwa mzito sasa, kundi zima linakuwa tu kama ukungu mkubwa mno, karibu unanifanya kipofu, huko mliko.

194 Hamuoni, kwamba hapa ishirini au thelethini, labda, wagonjwa, au zaidi, papa hapa kwenye jukwaa hili, na nje kwenye mkutano, kwamba Mungu hashindwi? Ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi kwa nini, kila Mzao wa Ibrahimu, mbona usichukue ufunguo sasa? Mshindi

mkuu, ambaye alishinda yote kwa ajili yako, yupo hapa. Yeye amethibitisha kwamba yupo. Unamwamini Yeye? [“Amina.”]

195 Basi chukua ufunguo wako wa imani, inua mikono yako, useme, “Yesu Kristo, ninaamini kwa uponyo wangu, sasa hivi.” Simameni kwa miguu yenu. Inueni mikono yenu, fungulieni imani yenu sasa. “Naamini, Bwana Yesu. Naamini sasa hivi.”

196 Sasa wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi. Weka mikono yako juu ya mwingine, Uzao mwingine wa Ibrahimu. Sasa muombee mtu huyo. Weka mikono yako juu yao. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

197 Shetani, umeshindwa vitani. Katika Jina la Yesu Kristo, ondoka hapa, na waache watu hawa waende zao, kwa utukufu wa Mungu.

MZEE IBRAHIMU SWA64-0207
(The Patriarch Abraham)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, Februari 7, 1964, katika Kern County Fairgrounds kule Bakersfield, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org